ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## WAJIBU WA KISHERIA WA KUSAJILI BIASHARA NA KUUNGANISHA MIFUMO YA TEHAMA NA MIFUMO YA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

**Zanzibar, 29, Agosti 2025.**

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inapenda kuwatangazia watu wote, Kampuni, na Taasisi nyingine zinazofanya shughuli za biashara ndani ya Zanzibar, ikiwemo wale wanaofanya **biashara kupitia majukwaa ya kidijitali au kutoa huduma za Malazi**, kwamba wanatakiwa rasmi:

(a) Kusajiliwa kama Walipakodi, na

(b) Kuunganisha mifumo yao ya TEHAMA na ile ya ZRA.

Matakwa haya yamewekwa wazi chini ya Kifungu cha 4A(5) na **Kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi Na. 7 ya mwaka 2009**. Vifungu hivi vipya vinaeleza kwa kina pamoja na hatua za kisheria zitakazochukuliwa endapo kutakuwa na kutokuzingatia masharti haya.

**Muongozo wa Utekelezaji:**

**Hatua ya 1: Kusajili kama Mlipa Kodi:**

Unaweza kukamilisha Usajili kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Walipakodi ya ZRA: **https://portalzidras.zanrevenue.org**. Huduma hii inapatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki, na ni rahisi kutumia popote Duniani.

**Hatua ya 2: Uunganishaji wa Mifumo:**

Walipakodi waliopo pamoja na wale watakaojisajili kuanzia tarehe ya tangazo hili, watalazimika kuunganisha mifumo yao ndani ya siku **thelathini (30)** Kutoka Siku ya Tangazo hili.

Kwa kwa msaada au maelezo zaidi kuhusu uunganishaji wa mifumo tafadhali wasiliana na ZRA kupitia;

- **Barua pepe**: ict.zra@zanrevenue.org
- **Simu:** +255 772 686 890 / +255 777 124 882

ZRA itaendelea kuhakikisha mazingira ya Ulipaji Kodi yanakuwa yenye Uwazi, Haki, Ufanisi na Rahisi ili kusaidia ukuaji wa biashara za Ndani na za Kimataifa sambamba na kuhakikisha Sheria za Nchi zinazingatiwa.

Imetolewa na:

**Kamishna Mkuu**